



OFISI YA MWANASHERIA  
MKUU WA SERIKALI



WIKI HII KWENYE  
NA MAGAZETI MITANDAO


26/08/2024

30/08/2024

OAG

# DAILY NEWS

28 & 29 /08/2024



NEWLY appointed Attorney General, Hamza Johari takes an oath of allegiance in Parliament before the Speaker Dr Tulia Ackson in Dodoma, yesterday. (Photo by Fadhilli Akida)



PRIME Minister,  
Kassim Majaliwa  
speaks to Attorney  
General, Hamza  
Johari in the  
National Assembly,  
in Dodoma,  
yesterday. (Photo by  
Fadhilli Akida)

Scanned with CamScanner

01



oagtanzania



www.oag.go.tz

## AG Johari aapishwa Bungeni na Spika

Na Joyce Kasiki, Dodoma

■■■ MWANASHERIA Mkuu wa Serikali (AG) Hamza Johari, ameapishwa na Spika wa Bunge Dkt. Tulia Ackson, kuwa Mbunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano .

AG Johari aliapishwa jana Bungeni jijini Dodoma mapema kabla ya kuanza Kikao cha kwanza cha Mkutano wa 16 wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.


Mwanasheria Mkuu wa Serikali amepishwa kwa mujibu wa Ibara ya 59(5) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya 1977 inayompa Mamlaka ya kuwambunge na kuhudhuria vikao vya Bunge.

Vilevile mara baada ya uapisho huo Mwanasheria Mkuu wa Serikali alikabidhiwa nyaraka mbalimbali za kumuwezesha kufanya kazi akiwa Bungeni na Spika wa Bunge I Dkt. Tulia Ackson.


Kuapishwa kiapo cha uaminifu mbele ya Bunge kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali ni kufuatia uteuzi uliofanywana Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kumteua Hamza Johari kuwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali mnano Agosti 15, 2024 na kufuatia na uapisho uliofanyika Agosti 16 ,2024 ikulu Jijini Dar es Salaam.

AG Johari ,amechukua nafasi ya Jaji Dkt. Eliezer Feleshi ambaye ameteuliwa kuwa Jaji wa Mahakama ya Rufani.

Kabla ya kuteuliwa kuwa mwanasheria Mkuu wa Serikali , AG Johari alikuwa Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Usafiri wa Anga (TCCA).



Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Hamza Johari akila kiapo cha uaminifu mbele ya Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Tulia Ackson, jana. Johari ameapa kabla ya kuanza Kikao cha Kwanza cha Mkutano wa Kumi na Sita wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. (Na Mpigapicha Wetu)



Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson akimwapiisha Hamza Johari kuwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali (AG), wakati wa mukutano wa 16 wa-Bunge, jijini Dodoma jana.

**PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

## Mwanasheria Mkuu mpya ala kiapo bungeni

Na Paul Mabeja, DODOMA

MWANASHERIA Mkuu wa Serikali (AG), Hamza Johari, amekula kiapo cha uaminifu mbele ya Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson.

Johari, alikula kiapo hicho muda mfupi kabla ya kuanza kikao cha kwanza cha Mkutano wa

16 Bunge la 12 jijini hapa.

Aliapishwa kwa mujibu wa Ibara ya 59 (5) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya 1977 inayompa mamlaka ya kuwa mbunge na kuhuduria vi-kao vya Bunge.

Baada ya kula kiapo, mwanasheria huyo mkuu wa serikali, alikabidhiwa nyaraka za kum-

wezesha kufanya kazi akiwa Bungeni na Spika.

Kiapo hicho cha uaminifu mbele ya Bunge kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, kinafuatia uteuzi uliofanywa na Rais wa Samia Suluhu Hassan Agost 15, mwaka huu na kuapishwa Agost 16 ikulu jijini Dar es Salaam.

Johari aliteuliwa kuwa AG

baada ya Jaji Dk. Eliezer Mbuki Feleshi aliyekuwa akishikilia wadhifa huo kuteuliwa na Rais Samia kuwa Jaji wa Mahakama ya Rufani.

Kabla ya uteuzi huo, mwanasheria huyo mkuu wa serikali alikuwa Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Usafiri wa Anga nchini (TCCA).

# AG Johari ala kiapo mbele ya Spika

Ja Gloria Tesha, Dodoma

**M**WANASHERIA Mkuu wa Serikali (AG), Hamza Johari meapa kiapo cha uaminifu nbele ya Spika wa Bunge, Dk 'Julia Ackson.

Mwanasheria Mkuu wa Serikali si mbunge lakini ni sehemu ya Bunge kwa mujibu wa sheria etu.

Johari alikula kiapo baada ya Vimbo wa Taifa na wa Afrika Mashariki kuimbwa na dua ya uanza shughuli za Kikao cha Wanza cha Mkutano wa 16 wa unge la 12.

Wakati akiapa alilieleza Bunge kuwa, atakuwa mwaminifu kwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

"Nitatumikia kwa nguvu zangu zote na kwamba nitai-hifadhi, nitailinda na kuitetea Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa mujibu wa sheria iliyowekwa, ewe Mwene-nyezi Mungu nisaidie," alisema Johari na baada ya hapo Dk Tulia alimkabidhi nyaraka.

Agosti 14 mwaka huu, Rais Samia Suluhu Hassan alimteua Johari awe Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Kabla ya uteuzi huo Johari

alikuwa Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Usafiri wa Anga (TCAA) na anachukua nafasi ya Dk Eliezer Feleshi ambaye aliteuliwa kuwa Jaji wa Mahakama ya Rufani.


Aidha wakati wa kikao hicho, Dk Tulia alitoa taarifa ya Spika ya kumuapisha Mahmoud Thabit Kombo kuwa mbunge baada ya Rais Samia kumteua Julai 10 mwaka huu kuwa mbunge na kisha kuwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki.

Alisema, kanuni ya 30 fasiri ya 2 B ya Kanuni za Kudumu za Bunge inampa mamlaka Spika

kumuapisha mbunge wakati hakuna mukutano wa Bunge unaoendelea na kisha kutoa taarifa bungeni katika kikoa cha kwanza cha mukutano.

"Napenda kutoa taarifa kwamba Mahmoud Thabit Kombo aliapa kiapo cha uaminifu siku ya Alhamisi Julai, 2024 katika Ofisi Ndogo ya Bunge, Dar es Salaam," alisema Spika.

Dk Tulia alimponeza Kombo na akamkaribisha katika Bunge na alimtakia heri katika utekelezaji wa majukumu alioaminiwa na Rais Samia kuwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki.



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa akibadilishana mawazo na Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Hamza Johari (kushoto) bungeni mjini Dodoma jana. (Picha na Fadhili Akida).



## CONTACT:

phone: +255 713 410 676  
+255 755 333 372  
P.O BOX 78392, Dar es Salaam  
Email. johnbukuku@gmail.com

Home Blashara Burudani Magazeti Mchanganiko Michezo Siasa Teknolojia TV Makala

Q Aa1 ☼

MCHANGANYIKO


## MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI ALA KIAPO CHA UAMINIFU BUNGENI



Alex Sonna · 3 days ago

Last updated: 2024/08/27 at 12:37 PM

Share f t e m



05



This Space can  
Only be yours

Call us today on  
+255 754 271 266

Home > HABARI > MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI AAPISHWA BUNGENI JIJINI DODOMA >

## MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI AAPISHWA BUNGENI JIJINI DODOMA

▀ MICHUZI BLOG □ AT TUESDAY, AUGUST 27, 2024 □ HABARI,

Na MWANDISHI wetu Bungeni - DODOMA

Mwanasheria Mkoo wa Serikali Bw. Hamza Johari amekula kiapo cha uaminifu mbele ya Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Tulia Ackson, tarehe 27 Agosti 2024. Mwanasheria Mkoo ameapa kabla ya kuanza kikao cha kwanza cha Mkutano wa kumi na sita (16) wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mhe. Mwanasheria Mkoo wa Serikali amepishwa kwa mujibu wa Ibara ya 59(5) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya 1977 inayompa Mamlaka ya kuwa mbunge na kuhudhuria vikao vya Bunge. Vilevile mara baada ya uapisho huo Mwanasheria Mkoo wa Serikali alikabidhiwa nyaraka mbalimbali za kumuwezesha kufanya kazi akiwa Bungeni na Spika wa Bunge la Tanzania Mhe. Dkt. Tulia Ackson.


Aidha kuapishwa kiapo cha uaminifu mbele ya Bunge kwa Mwanasheria Mkoo wa Serikali kunafuatia uteuzi uliofanywa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan wa kumteua Bw. Hamza Johari kuwa Mwanasheria Mkoo wa Serikali mnano tarehe 15 Agosti 2024 na kufuatia na uapisho uliofanyika tarehe 16 Agosti 2024 Ikulu Jijini Dar es Salaam.

Mhe Mwanasheria Mkoo wa Serikali Bw. Hamza Johari amechukua nafasi ya Mhe. Jaji Dkt. Eliezer Mbuki Feleshi ambae ameteuliwa kuwa Jaji wa Mahakama ya Rufani, ambapo kabla ya kuteuliwa kwake kuwa Mwanasheria Mkoo wa Serikali, Bw. Hamza Johari alikuwa Mkurugenzi Mkoo wa Mamlaka ya Usafiri wa Anga (TCCA).



oagtanzania

⋮



[View insights](#)

[Boost post](#)



• • • • •



39 likes

oagtanzania MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI  
AAPISHWA BUNGENI JIJINI DODOMA... more

View all 0 comments

07



oagtanzania



[www.oag.go.tz](http://www.oag.go.tz)



oagtanzania

🎵 oagtanzania • Original audio

⋮



## MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI AAPISHWA BUNGENI

WELEDI NA UBORA

Kwa msaada wa huduma za Kisheria piga simu bure 0800 11 0188



[www.oag.go.tz](http://www.oag.go.tz)

OAG TV



@oagtanzania

X @oag\_tz



[View insights](#)

[Boost post](#)

08



oagtanzania



[www.oag.go.tz](http://www.oag.go.tz)



oagtanzania and officialtcaa

:



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI



Bw. James Cletus Mshanga

## SALAMU ZA POLE

Mwanasheria Mkuu wa Serikali Mhe. Hamza S. Johari anatoa salamu za pole kwa Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa Mamlaka ya Usafiri wa Anga Tanzania (TCAA), Menejimenti ya TCAA na Watumishi wote kufuatia kifo cha Mtumishi wa TCAA Bw. James Cletus Mshanga (Dereva Mwandamizi) kilichotokea tarehe 28 Agosti, 2024, Moshi, Kilimanjaro.

**MUNGUA ILAZE ROHO YA MAREHEMU  
MAHALA PEMA PEAPONI, AMINA.**



WELEDI NA UBORA



[www.oag.go.tz](http://www.oag.go.tz) OAG TV @oagtanzania @oag\_tz

[View insights](#)

[Boost post](#)

09



oagtanzania



[www.oag.go.tz](http://www.oag.go.tz)



OAG Tanzania

14h ·

...

Bunge lapitisha Muswada wa Sheria ya  
Marekebisho ya Sheria ya Hifadhi ya Jamii ya  
Mwaka 2024



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI



Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya  
Hifadhi ya Jamii wa Mwaka 2024 Umepitishwa na  
Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

29/08/2024

Kupakua Muswada huu, Tumia Kikoa ([link](#)) hapa chini



<https://oagmis.agctz.go.tz>

Weledi na Ubora



[www.oag.go.tz](http://www.oag.go.tz)



OAG TV



@oagtanzania



@oag\_tz

See insights and ads

Boost post

10



[oagtanzania](#)



[www.oag.go.tz](http://www.oag.go.tz)



# TUPO KARIBU YAKO!

## Tufuatilie kupitia ✅



[oagtanzania](#)



[info@oag.go.tz](mailto:info@oag.go.tz)



[www.oag.go.tz](http://www.oag.go.tz)

Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali  
Mtaa wa Mtumishi  
Mji wa Serikali Mitumba  
S. L. P 630  
Dodoma - Tanzania

KWA MSAADA WA HUDUMA ZA KISHERIA PIGA SIMU BURE 0800 11 0188

Weledi na Ubora